**MKATABA WA KUPANGISHA CHUMBA NA: 2 KILICHOPO FLAT NA: 05 WING B KIWANJA NA: 366/57 MTAA WA SAMORA NA ZANAKI DAR ES SALAAM**

19 JAN 2026
REAL ESTATE
TAX REGION

**MKATABA HUU** umefanyika tarehe **20/01/2026**

**KATI YA**

**BULALI HAMISI BULALI** akiwa mtu binafsi wa **S.L.P 36470** Dar es salaam (ambaye ndani ya mkataba huu atajulikana kama mwenye nyumba) wa upande mmoja

NA

**MR ATHA AMINIELY SWAI** akiwa ni mkurugezi **S.L.P 38415 DAR ES SALAAM** kwa niaba ya **AMANI QUICK DELIVERY T LIMITED** (ambaye ndani ya mkataba huu kama mpangaji wa upande mwingine)

Kwa kuwa mwenye nyumba ndie mmliki mtarajiwa wa **FLAT** na.**05 WING B** kiwanja na: **366/57** iliyoko kwenye makubaliano ya samora na zanaki Dar es salaam.

**MKATABA UNASHUHUDIWA MAKUBALIANO YAFUATAYO KATI YA MWENYE NYUMBA NA MPANGAJI**

1. Kwamba mpangaji anapanga chumba na:01(room) chenye ukubwa wa **SQUARE METERS 3** kwa ajili ya ofisi (ambayo inajulikana kwenye mkataba huu kama chumba)
2. Mkataba utakuwa wa mwaka mmoja kuanzia leo terehe **20/01/2026** na utamalizika **20/01/2027** Kodi ya chumba kwa mwezi ni **300,000**
3. Mpangaji haruhusiwi kupangisha mtu mwingine bila idhini ya mwenye nyumba
4. Mpangaji ataweka chumba katika hali ya usafi ndani na nje na hataruhusiwa kukifanyia matengenezo wala kukibadili muundo wake bila idhini/ruhusa ya mwenye nyumba
5. Mpangaji atalipa gharama ya maji, umeme na usafi kipindi ambacho atakaa kwenye chumba husika
6. Mpangaji atamruhusu mwenye nyumba kuingia ndani ya chumba husika na kuangalia hali halisi ya chumba au kukifanyia ukaguzi baada ya kupokea taarifa ya ubovu au uharibifu kutoka kwa mpangaji
7. Endapo mpangaji atapenda kuendelea kupanga chumba baada ya kumalizika kwa mkataba inabidi kutoa taarifa kwa mwenye nyumba wiki moja kabla ya mkataba kumalizika. Endapo hata fanya hivyo mwenye nyumba atachukulia kuwa hana nia ya kuendelea
8. Uharibifu utakao tokea kwenye chumba utakao sababishwa na mpangaji matengenezo yake yatagharamiwa na mpangaji

9. Kodi ya ofisi ikicheleweshwa kulipwa kwa wakati wa mkataba kwa kupitisha muda wa miezi miwili bila sababu za msingi mkataba utavunjwa na mpangaji kuhamishwa

**MWENYE NYUMBA ATAFANYA YAFUATAYO**

(A) Matengenezo makubwa yatakayo hitajika katika chumba ambayo hayakusababishwa na mpangaji yatagharamiwa na mwenye nyumba

(B) Kodi ya kiwanja na malipo mengine yatagharamiwa na mwenye nyumba isipokuwa ushuru wa stempu ya mkataba huu ambao utalipwa na mpangaji,

**KWA USHUHUDA** wa makubaliano hayo pande zote mbili zimetia sahihi kwa ilivyo hapa chini

**Umetiwa sahihi na kusainiwa na**

JINA: BULALI HAMISI BULALI
Wadhifa: MWENYE NYUMBA
Tarehe: 19/01/2026

.................... **sahihi**

**Mwanasheria**
JINA: Deogratius Ogunde ogunde
Wadhifa: wakili
Tarehe: 19 January 2026

.................... **sahihi**

JINA: AITHA AMINIELY SWAI
Wadhifa: MKURUGENZI
Tarehe: 19/01/2026 .................... **sahihi kwa niaba ya**

**AMANI QUICK DELIVERY T LIMITED**

**Mwanasheria**
JINA: Deogratius Ogunde Ogunde
Wadhifa: wakili
Tarehe: 19 January 2026

.................... **sahihi**

TIN NO 105-955-020
TEL NO 0607545844441
WHT 360,000/:
SD 36,000/:
COPY 1500/:
Total 37,500/:

**STAMP DUTY**
Shs. 36,000/= Collected
Receipt No. 998412540876? Date: 19/1/2026

Regional Manager - Ilala Tax Region